# JOHN MERLINI SECONDARY SCHOOL

MISSIONARIES OF THE PRECIOUS BLOOD
P.O. Box 2010
**DODOMA – TANZANIA**

tel. 0766 939 536
e-mail: jmerlinisec@gmail.com
web-site: cppseducationtz.org

**Registration N° S 4880, NECTA Exams N° S 5391**


KWA MZAZI / MLEZI WA ……………………………………………………………………….

**YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2019**

**UTANGULIZI**

Uongozi wa shule unayo furaha kukujulisha kuwa mwanao amechanguliwa kujiunga na Form I katika Shule ya Sekondari John Merlini mwaka 2019. Shule ni ya mseto, wasichana na wavulana, na ya bweni. Itafunguliwa rasmi siku ya Jumatatu **tarehe 08/01/2018.**

**MALIPO:**

Malipo ya **ada ya shule, bweni na michango ni sh. 2,00,000**. Yaweza kulipwa kwa awamu moja (January 1, 2019); au kwa awamu mbili (January 1, sh. 1,000.000 na July 1 sh. 1,00.000) au kwa awamu tatu (January 1, April 1, July 1: kila awamu sh. 667,000). Lazima malipo yote yawe yamekamalika kwa tarehe 1 July, 2019. Malipo ya ada ya shule yafanyike kupitia benki ya NMB katika mojawapo ya account mbili zifuatazo:

- JINA LA BANK NMB
- JINA LA ACCOUNT: JOHN MERLINI SECONDARY SCHOOL
- NAMBA YA ACCOUNT: 52010026469

- JINA LA ACCOUNT: JOHN MERLINI SEC. SCHOOL DORMITORY
- NAMBA YA ACCOUNT: 52010031122

Mwanafunzi atapokelewa shuleni akionyesha tu ***pay in slip*** ya Benki iliyokamilika kwa awamu husika ya ada.

**MAHITAJI:**

| | |
|---|---|
| **Sare**: Suruali/sketi rangi ya kaki, shati jeupe, sweta rangi damu ya mzee. Zinapatikana shuleni zenye nembo ya shule kwa jumla ya sh 44,000 kwa pea | |
| Viatu vya ngozi rangi nyeuzi, Soksi nyeupe. Vyatu vya raba rangi nyekundu | |
| Truck suit 2: moja ya rangi nyekundu, na moja ya rangi ya blu, Vinapatikana shuleni kwa jumla ya sh. 50.000 | |
| T Shirt 2: moja rangi nyekundu, moja rangi ya blu | |
| Counter Books 13, Kalamu 2 za wino, Penceli 2, Kifuto 1, Mathematical set 1, Madaftari madogo ya mazoezi 13, Rula 1 | |
| 4 figure Mathematical Tables, Concise Swahili-English Dictionary | |
| Ream 1 ya karatasi A4 ya kuikabidhi ofisi | |
| Bima ya Afya NHIF, NSSF. Kama huna, shule itatengeneza kwa sh. 54,000 | |
| Sahani, Kijiko, Kikombe, fagio, mop ya kudekia, ndoo | |
| Kaptula na fulana kwa michezo na kazi | Vifaa vya usafi binafsi: sabuni ya kuogea, ya kufulia, dawa ya meno, mswaki, mafuta ya kujipaka |
| Sandals | |
| Mashuka 2 ya rangi ya pink kwa wasichana | |
| Mashuka mawili rangi ya blu kwa wavulana | Begi la madaftari |
| Chandalua, mto, taulo | Mwanvuli |
| Kanga na kitenge kwa wasichana | Saa ya mkononi |
| Nguo za ndani | Trunk ya chuma kuhifadia vitu binafsi |
| Kiwi nyeusi | |

**Ni lazima kufuma kwa nyuzi au kuandika kwa wino usiofutika na herufi kubwa jina zima la mwanafunzi juu ya nguo zake zote**

**MWONGOZO KWA MWANAFUNZI**

1. Lengo la shule ni kumpatia mwanafunzi elimu bora na kumjenga kitabia na maadili ambayo yatamwezesha awe raia mwema. Naye mwanafunzi anatakiwa kuweka masomo mbele na kufuata kiaminifu sheria za shule na za bweni ambazo zitamsaidia kufikia mafanikio mazuri na malengo ya shule.
2. Lugha ya mawasiliano shuleni ni kiingereza tu ya kutumika kila wakati.
3. Mmiliki wa shule anapanga ada baada ya kusikiliza bodi ya shule. Kutolipa au kuchelewa kulipa ada kwa wakati unaotakiwa kutasababisha kusimamishwa au kuachishwa shule au kunyimwa kufanya mtihani.
4. Maktaba ya shule ina vitabu kwa wanafunzi kuvitumia, lakini havitoki nje ya maktaba. Wazazi/walezi wanashauriwa kumnunulia mtoto wake vitabu vyake binafsi vya kujisomea.
5. Mabweni yanafungwa asubuhi saa 1:00 na kufunguliwa tena saa 11:30 jioni. Mwanafunzi akitoka bwenini asubuhi kwenda darasani awe amechukua vifaa vyote anavyovihitaji kwa siku hiyo. Hataruhusiwa kurudi bwenini wakati wa masomo.
6. Siku zisizo za shule (jumamosi mchana, jumapili na sikukuu zingine) wanafunzi watapewa nafasi ya kujihusisha na shughuli zingine kama vile debating clubs, theatre, talents show, sports, seminars, nk. Dhumuni ni kumpa kila mwanafunzi uwezo wa kukuza na kuweka hadharani karama zake.
7. Mwanafunzi ana jukumu la kufanya usafi kila siku shuleni na bwenini katika muda unaotolewa.
8. Vitu vya shule na vya bweni vipo hali sawa. Anayeviharibu anagharimiwa utengenezaji wake.
9. Mazingira ya shule na ya bweni daima yawe ya utulivu. Kuacha darasa la kusomea, kupiga kelele, kufanya shughuli tofauti hakuruhusiwi.
10. Mgeni haruhusiwi kuingia katika vyumba vya kulala wanafunzi bali anakaribishwa mahali anapoonyeshwa na matron/patron.
11. Mwanafunzi haruhusiwi kuenda nyumbani wakati wowote wa muhula wa masomo isipokuwa kwa sababu maalum. Ruhusa inatolewa na mkuu wa shule tu.
12. Kila asubuhi na jioni wote kwa pamoja watasali sala ya asubuhi na jioni. Kila jumapili wote watahudhuria ibada ya kikristu (kikatoliki) inayoadhimishwa katika ukumbi wa shule.
13. Mwanafunzi anashauriwa kutobaki na fedha binafsi bwenini bali aikabidhi kwa Shemasi Hillary Ngowi, ambaye atampatia mwanafunzi kila atakapoihitaji. Uongozi wa shule hautawajibika juu ya upotevu wa fedha ambayo hakukabidhiwa Shemasi.
14. Mzazi/Mlezi anayemtumia hela mtoto wake kwa sababu yoyote atume kwa mhusika tu ambaye ni Shemasi Hillary Ngowi.
15. Mzazi/Mlezi daima adai risiti ya shule kwa fedha zote ambazo analipia shuleni na alipe kwa wahusika tu ambao ni Mwalimu Mkuu na Shemasi Hillary Ngowi

**MWENENDO WA MWANAFUNZI**

Jarida linaloitwa STUDENTS HANDBOOK 2018 linaonyesha wazi taratibu zote ambazo zinamwongoza mwanafunzi akiwa shuleni na bwenini.

Hizi zifuatazo ni baadhi ya taratibu:

a) “Mtendee mwezako kama unavyopenda kutendewa wewe” Maneno haya ya Yesu ni mzizi wa uelewa wa J. Merlini, inayowataka wanafunzi kupendana, kuheshimiana na kuthaminiana.

b) Mwanafunzi awe na adabu njema ndani na nje ya shule, mkweli, mtiifu na mwenye heshima kwa walimu, patron/matron, wafanyakazi na wanafunzi wenzake shule. Apokee maelekezo na maagizo anayotolewa bila ubishi.

c) Aonyeshe moyo mwema wa kuwasaidia wanafunzi wenzake wasio na uwezo sawa na yeye. Afuate motto wa shule unaosema: “EDUCATION FOR SERVICE IN SOLIDARITY”.

d) Ajitenge na makosa yafuatayo: ugomvi wa kupigana, lugha ya matusi au ya kutisha, wizi au uharibifu wa mali ya shule na ya wengine, udanganyifu, unyanyasaji wa kijinsia, ubakaji, uhusiano wa kimapenzi, kumpa mimba, kupata mimba, kutoa au kushiriki kutoa mimba, kumiliki na kutumia madawa ya kulevya, kutoka nje ya eneo la shule na bweni bila ruhusa, kuiba mitihani.

e) Asiwepo shuleni na bwenini na simu ya mkononi wala radio ya mfukoni. Akihitaji kupiga au kupigiwa simu na wazazi/walezi itatumika simu ya shule. Kwa jumla taarifa kutoka nyumbani zinatolewa kwa kupitia uongozi wa shule na sio kwa mwanafunzi husika moja kwa moja.

f) Sare ya kubana au fupi hairuhusiwi. Asivae urembo wa aina yoyote.

**Ili shule iweze kufikia malengo yake, na kujipatia sifa ya kitaaluma na kinidhamu, ushirikiano mzuri uwepo kati uongozi wa shule, walimu, wafanyakazi, wanafunzi na wazazi /walezi.**